

Tathmini ya Mfumo wa Kitaasisi wa Maboresho wa Utumishi kwa Umma

Uchunguzi wa Kina wa Ushirikishaji wa Wananchi Kwenye Huduma za Maji Safi na Maji Taka nchini Tanzania

Na: Jamal Msami

Utangulizi

Muhtasari huu unatoa taswira fupi ya tathmini ya mchango wa ushirikishwaji wa wananchi katika mifumo badilifu ya utoaji wa huduma za maji safi na maji taka (WATSAN) nchini Tanzania. Tathmini hii imefanyika katika wakati muafaka ambapo pamoja na kuwa na zaidi ya muongo mmoja wa utekelezaji wa maboresho ya sera ya maji, machache yanafahamika kuhusu: Mosi, namna ambavyo wananchi wanashiriki kwenye michakato ya utengenezaji na utekelezaji wa maboresho ya huduma; na *Pili*: mchango ambao jamii unatoa kwenye utoaji wa huduma husika. Taswira hii inatokana na kitabu kilichojikita kwenye uchunguzi wa kina wa huduma za Maji Safi na Maji Taka uliofanyika katika kata ya Kawe, manispaa ya Kinondoni, nchini Tanzania. Utafiti ulitumia fasihi na maandishi mbali mbali kuhusu maboresho ya utumishi wa umma, ushirikishaji wa wananchi na nadharia ya kihistoria ya mfumo wa kitaasisi, katika kuwasilisha na kuchambua kwa kina utekelezaji wa dhana na sera ya ushirikishwaji wa wananchi, mahusiano kati ya watendaji wa kitaasisi na wananchi kwenye utengenezaji na utekelezaji wa maboresho ya sera utoaji wa huduma za maji safi na maji taka katika eneo la tafiti husika.

Utafiti huu ulitumia data msingi na data fuatizi. Zoezi la ukusanyaji wa data za msingi katika utafiti huu lilifanyika uwandani, yaani mahali palipofanyiwa utafiti, kati ya mwezi Machi na Julai mwaka 2014. Ukusanyaji wa data fuatizi ulifanyika kati ya mwezi Januari 2014 na mwezi Aprili 2017. Mtafiti alitumia njia tatu katika kukusanya data za utafiti huu. Njia hizo ni usaili, hojaji na maktabani. Mtafiti aliteua njia hizi kwa sababu ndizo zilizofaa zaidi katika uchunguzi wa mada yake ili kupata data zilizo thabiti kuliko njia nyingine kama vile ushuhudiaji na ushiriki.

Kwa ujumla utafiti ulibainisha mambo makuu mawili:

- *Moja*, Kukosekana kwa ufasaha kwenye maagizo ya sera kuhusu ushirikishwaji wa wananchi kwenye maboresho ya huduma za Maji Safi na Maji Taka. Mkanganyiko wa maandiko na maudhui ya sera unatoa mwanya wa tafsiri shindani na kinzani katika utekelezaji wa sera jambo ambalo linasababisha matokeo mchanganyiko ya utekelezaji wa sera.
- *Mbili*, Usanifu wa maboresho ya sera ya Maji Safi na Maji Taka unabainisha uwepo wa mapungufu ya tathimini shirikishi ya uhalisia wa mazingira tekelezi yenye kuathiri utekelezaji wa sera.

Matokeo ya utafiti huu yanatoa mchango mpya na wa kipekee kwenye taaluma ya maboresho ya

utumishi wa umma, pamoja na fasihi juu ya ushirishwaji wa wananchi. Mchango huu unatokana na uchambuzi wa kina wa mazingira halisi na changamoto za utekelezaji wa maboresho ya ushirikishwaji wa wananchi katika huduma za Maji Safi na Maji Taka. Utafiti unapendekeza kwamba kuna haja ya wadau hasa mamlaka za dola kupitia na kutathmini upya taasisi na taratibu za ushirikishwaji wa wananchi ili kuondoa mkanganyiko kwenye utekelezaji wa sera. Hili linaweza kufanyika kwa kuboresha uwazi, ubayana na uwezeshaji kwenye taratibu hizo ili kuharakisha mafanikio tarajiwa kwenye sekta ya maji safi na maji taka.

Msingi na Lengo la Utafiti Uliofanyika

Dhana ya ushirikishaji wa wananchi (UW) inahusiana na uwezo wao kuchangia kikamilifu kwenye usanifu, utengenezaji, utekelezaji na ubora wa sera. Dhana hii inajengwa na imani ya kwamba ushirikishaji wa wananchi huwawezesha wadau mbalimbali kuunganisha nguvu kwenye kutatua fursa na vikwazo wanavyokumbana navyo. UW umejitokeza kuwa mhimili katika maboresho ya mfumo wa kitaasisi kwenye sekta ya Maji Safi na Maji Taka (WATSAN) ambayo madhumuni yake ni kuboresha utoaji wa huduma kwa umma. Ujumuishaji wa dhana ya UW kwenye maboresho ya mifumo ya WATSAN ni kielelezo cha Tanzania kukubaliana na vigezo vya ufanisi na njia bora kama zilivyoielezwa kwenye Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs) Lengo la 8, na sasa kwenye Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) Lengo namba 16, ambayo yanasisitiza mashirikiano kati ya wadau kwenye maamuzi ya maendeleo na ukuzaji wa jumuiya za maendeleo.

Kiini na dhamira ya UW kwenye sera na maboresho ni mvuto utokanoa na ubinadamu na manufaa yanayoweza kupatikana na kuboresha mifumo na taratibu za uongozi na pia kuleta matokeo yanayo imarisha haki na usawa (Barnes n.w., 2014). Fikra ya msingi ni kwamba kwa kuwashirikisha wananchi, washiriki huweza kupata matokeo na manufaa ambayo wasingeyapata endapo kila mdau angetenda peke yake.

Ili kuenzi na kijifunza njia bora za kimataifa za kufanikisha jitihada za maendeleo, Tanzania imeridhia na kutia sahihi mikataba mbalimbali ya kimataifa kuhusu hizo njia bora na pia imerekebisha sera na mifumo yake kwenye maeneo ya WATSAN ili kuhimiza ongezeko la UW kwenye utoaji wa huduma, ahueni ya gharama, ung'atuzi wa usimamizi na pia utengenezaji wa mikakati ya utekelezaji na usimamizi jumuiishi (Doering, 2005; URT, 2002). Tanzania imepanua wigo wa UW kwenye WATSAN husuasani kwa lengo la kukusanya raslimali ili kukabili tatizo la gharama zinazoambatana na kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma, utengenezaji wa mazingira endelevu ya mifumo ya kuzuia madhara na maafa yatokanayo na maji, kwa mfano mafuriko na ukame na kuimarisha uswa katika utoaji wa huduma (URT, 1991, 2002). Tarajio kubwa limekuwa kwamba maboresho ya huduma za WATSAN yatazaa matunda kwenye maeneo mengi ya kiuchumi na kijamii ikiwemo pia kupunguza athari za kiafya, na kuchagiza ongezeko la tija na mapato yatokanayo na ajira na kazi.

Hata hivyo, pamoja na utekelezaji wa maboresho ya mifumo ya WATSAN kwa takribani miongo miwili, bado kuna utata kwenye ushahidi ulioko kuhusu mafanikio ya mabadiliko haya ya kisera. Kwa upande mmoja, ujenzi umeanza wa mfumo wa udhibiti wa kiutendaji

(yaani sheria, sera, na mikakati) pamoja na ule wa taasisi. Ujenzi huu umeshuhudia na kuongozwa na sera mpya mbili za maji, mabadiliko ya kisheria kuhusiana na WATSAN (hususani maji na mazingira safi kwa afya), na mikakati maridhawa ya utekelezaji inayoambatana na sheria za usimamizi huru wa utoaji wa huduma. Kwa upande mwingine viashiria vya utendaji kuhusu upana na upimaji wa matumizi ya huduma vinaonyesha mafanikio finyu kwenye eneo la huduma za maji na ukosefu wa maendeleo kwanya eneo la mazingira safi. Kati ya mwaka 1990 na 2012, takwimu za viashiria vya kupima huduma za maji taka na mazingira zilibakia zile zile, yaani robo ya jumla ya watu wote nchini. Mathalani, takwimu za viashiria vya usambazaji wa huduma na matumizi ya maji safi kwa ujumla ziliongezeka toka 56% hadi 65% (NBS, 2014; URT, 2012ca; [Water and Sanitation Program, 2011](#)).

Haya matokeo kanganyifu yanaashiria jambo ambalo kwenye uchanganuzi wa sera hujulikana kama 'maboresho hadaa' au 'signalling' kwa lugha Kiingereza ([Andrews, 2013, pp. 28-9](#)). *Maboresho hadaa* au *Signalling* hutokea pale ambapo maboresho ya sera hufanyika kwa madhumuni ya kutoa hisia kwamba mamlaka inafanikiwa kwenye malengo yake ya muda mfupi. Mara nyingi lengo huwa ni kuvutia misaada ya kifedha na kujiongeza uhalali wa kisiasa, na siyo kuimarisha umadhubuti wa suluhisho la tatizo husika la kisera. Tathmini liyofanywa mwaka 2012 na Wizara ya Maji ya maboresho ya WATSAN nchini Tanzania inaashiria ya kwamba utekelezaji wa dhana ya UW unaathiriwa na ombwe la malengo yenye mashiko, mwongozo kuhusu jinsi ya kuwashirikisha wananchi, utaratibu wa mgao wa raslimali muhimu na utaratibu wa kuratibu na kutathmini utendaji. Sambamba na hisia za mapungufu kwenye utekelezaji wa sera za maboresho, kumekuwa na utata pia kuhusu hatua zilizochukuliwa kutanua wigo wa ushirikishaji wananchi katika WATSAN. Pamoja na kuongezeka kwa jitihada za ushirikishaji wananchi, tafiti za maoni zinaonyesha kwamba idadi ya wananchi wanaoridhishwa na jinsi Serikali inavyoendesha WATSAN imeshuka toka 46% mwaka 2002 hadi 34% mwaka 2012 (Afrobarometer, 2003, 2012).

Kutokanana matokeo haya kanganyifu, ni dhahiri kwamba ushirikishaji wa wananchi kwenye maboresho ya WATSAN haujafikia malengo yake au kutoa matokeo yaliyotarajiwa. Nia ya utafiti huu ilikuwa kufuatilia hisia hizo ili kuongeza uelewa wa kiini cha mapungufu haya. Kwa hiyo utafiti ulijikita kwenye kuchunguza maswala mawili: kwanza kwa kuungalia mfumo wa usimamizi na uwezeshaji wa ushirikishaji wa wananchi, na pili kwa kutathmini mchango wa wa ushiriki wa wananchi kwenye utoaji wa huduma husika. Ili kufikia malengo haya mawili, utafiti ulijikita kwenye sekta ya Maji Safi na Maji Taka (WATSAN) ili kufanikisha uchanganuzi wa miundo ya mfumo

na uwiano wa taasisi mbali mbali na mchakato mzima wa ushirikishaji wa wananchi. Katika tathmini ya ushirikishaji wa wananchi, utafiti uliangalia kwa undani mahusiano kati ya wananchi na vyombo na taasisi mbali mbali za serikali na kuchunguza uzito wa mchango wa wananchi katika maamuzi yanayohusu utoaji kwa umma za Maji Safi na Maji Taka. Utafiti ulitilia mkazo utekelezaji wa sera ya UW katika kipindi kati ya mwaka 2002 na 2013, kipindi ambacho kilitumiwa kutekeleza maboresho kwenye utoaji wa huduma kwenye sekta ya WATSAN amabayo yalizingatia sera ya ushirikishaji wa wananchi kwenye maamuzi yanayohusu utekelezaji wa sera husika.

Hususani, utafiti huu ililenga kupata majibu ya maswali mawili wa msingi:

1. *Je ni namna gani mfumo wa taasisi na mchakato wa ushirikishaji unaathiri au kuimarisha ushirikishaji wa wananchi kwenye WATSAN?*
2. *Je ni namna gani UW unaboresha au kuathiri utoaji wa huduma za WATSAN?*

Ili kupata majibu ya maswali haya utafiti ulijikita kwenye kuchunguza uwiano na mahusiano kati ya wananchi na taasisi simamizi za magaeuzi yenye lengo ya ushirikishaji wa wananchi kwenye WATSAN.

Matokeo ya Utafiti

Katika kujibu ya swali la kwanza— *Je ni namna gani muundo na mfumo wa taasisi na mchakato wake vinaathiri au kuimarisha ushirikishaji wa wananchi?* – matokeo yanaonyesha kuwa taasisi kama hizi zinaweza kuwezesha ushirikishaji wa wananchi kwa kutoa haki na majukumu na pia hadhi na wajibu na pia ridhaa na mamlaka (Scott, 2013a, uk. 64). Vigezo hivi huweza kuboresha au kuathiri jinsi gani watendaji mbali mbali wanavyotumia au kutafsiri kanuni na hiyo huweza kupunguza au kuongeza tija ya mabadiliko. Hali halisi ya taasisi huathiri au kuboresha uwezekano wa kupitishwa au kukubalika na pia uhalali wa ushirikishaji. Kiuhalisia kwa sasa mfumo kabambe wa usimamizi upo lakini pia unatekelezwa sambamba na tafsiri shindani na kinzani za sera ambazo zinaathiri ufikiaji wa malengo ya sera. Uwezo wa kanuni hizi kinzani zisizokuwa rasmi kuathitiri malengo yaliodhamiriwa huonekana bayana pale ambapo mamlaka na madaraka ya kusimamia ushirikishaji hukasimiwa ukisaidiwa na mfumo hafifu wa usimamizi, ufuatiliwa na uhimizaji wa utendaji sahihi kwenye tasasisi. Matokeo yake huwa ni kupotosha aina ya manufaa na maslahi yatokanayo na ushirikishaji wa wananchi na hii huleteleza washiriki kushiriki shingo upande au kuukubali bila kuuamini (Oliver, 1991). Matokeo ya utafiti yanaonyesha pia kwamba kuna upinzani wa kichinichini kuhusu ushirikishaji wa wananchi kwenye WATSAN. Hizi ni dalili za kupungua kwa hamasa na kufurahia maboresho hasa kutokana na ukosefu wa mlingano kati ya wananchi kukubali mfumo wa ushirikishaji na matokeo ya ushirikishaji kwenye sehemu mbali mbali za mfumo wa UW. Jitihada za ziada wakati wa kutengeneza dhana ya kuongoza utafiti ili kupambanua kati ya muundo wa taasisi na ushiriki wa watendaji hazikufanikiwa.

Kwa ujumla matokeo ya utafiti yanaashiria kwamba taasisi wa mifumo isiyokuwa rasmi ambayo zimejikita kwenye taratibu na tamaduni za utendaji¹—ni vielelezo vya msingi kuhusu kufanikiwa

¹ Msoshiojia William Richard Scott ametoa rai kwamba utambuzi wa vipengele vya utamaduni argues that vipaji vya kutambua vipengele vya utamaduni hujitokeza kwenye itikadi na miongozo ya taasisi amabayo inatokana na makundi ya jamii na imani zao kama dini, utaiifa, na lugha (Scott, 2013). Vitu hivi hutoa kiolezo cha tafsiri ya mazingira ya taasisi na jinsi ya kupokea, kuchanganua na kutafuta maana ya taarifa. Kwa upande wake vipengele vya kanuni huhusu mila na desturi zilizojitika katika jamii. Hizi hutoa vigezo vya yanayokubalika na yaliyo sahihi kwenye. Kanuni hujenga tabia za watu binafsi kwa kuwafanya wapate hisia za heshima au

au kushindwa kwa UR kwenye WATSAN. Kanuni na taratibu kwenye jamii na taasisi hujenga tabia za watendaji na tafsiri zao za maana na madhumuni ya UW (Oliver, 1991). Taratibu hizi ambazo zinaweza kuathiri au kuendeleza malengo ni kielelezo kikubwa kuhusu kiwango ambacho mtendaji binafsi au na wenzake, anaweza kufuata, kukaidi au kugushi matokeo ya shughuli zake. Inatia wasiwasi pia kwamba katika mabadiliko yatokanayo na maboresho kwenye WATSAN, hakuna uelewa wa pamoja kuhusu dhamira na maana ya UW kwenye jamii. Hii inaletwa na changamoto zitokanazo na mtafaruku unaozua kukubalika na kupokelewa kwa UW kwa sababu taasisi na jamii zinaonekana zinatumia taratibu zitokanazo na hadidi rejea na nyaraka tofauti. Hii inatengeneza mazingira sahihi kwa kundi lolote la watendaji wenye nia ya kubadili mfumo na taratibu za WATSAN. Andrews (2013) na Peters na Pierre (2016) wameshauri kwamba katika mangira kama haya mabadiliko na maboresho ya ziada linaweza kuwa jambo zuri kwa sababu yanahitajika kuhakikisha kuna uwiano kati ya mihimili mitatu ya kitaasisi ili kuifanya ishabihiane na hali halisi na ielekeze kwenye mafanikio yaliyolengwa. Mabadiliko kama haya yanaweza kuongeza ufanisi kwenye aina na kiwango cha ushirikishaji wa wananchi na kuongeza chachu ya maboresho kwa ujumla.

Katika kujibu swali la msingi la pili— *Je namna gani UW unaboresha au kuathiri utoaji wa huduma za WATSAN?*—matokeo ya utafiti yanaonyesha kwamba lengo kubwa la maboresho kwenye WATSAN ni kuboresha utaoaji wa huduma. UW ni mbinu ya kuimarisha lengo hili kwa kuhimiza upatikanaji wa huduma, uwajibikaji wa taasisi husika na kuleta ahueni ya gharama. Hata hivyo, kutokana na baadhi ya watendaji wa WATSAN kutumia vibaya utata kwenye tafsiri ya kanuni

na taratibu, ushahidi kuhusu mchango unaotokana na ushirikishaji wa wananchi bado una utata. Kwa upande mmoja, kwa ngazi za juu UW umefanikiwa kuongeza uwajibikaji wa jamii kwa kuongeza mtiririko wa taarifa kati ya watoa huduma, mamlaka za wilaya na jamii. Hili limefanikisha ongezeko la utekelezaji wa sera za maboresho. Pia kuna maeneo ambako UW umesaidia jitihada za taaasisi za ngazi za juu kuboresha utoaji wa huduma. Ni dhahiri kwamba haya yametokea licha ya taarifa zinazoonyesha kwamba kiwango cha UW kilikuwa kidogo kwenye eneo la kusanifu miundo na mifumo ya utekelezaji na kusaidia kupunguza gharama za huduma za WATSAN.

Kwa upande mwingine, ingawaje maboresho yamekuwa yakitekelezwa kwa zaidi ya muongo mmoja, matokeo yenye mashiko kwenye maeneo ya Maji Safi na Maji Taka hayajawa ya kuridhisha. Licha ya msisimko na mwamko mkubwa kwenye jamii kuhusu UW, dhana hiyo imeshindwa kuboresha upatikanaji wa huduma za mazingira safi kwenye kata husika. Pale ambako huduma zimeboreshwa kwa mfano kwenye utoaji wa maji safi, mafanikio hayakutokana na mfumo rasmi wa ushirikishaji wananchi na hii imekuwa licha ya mchango mdogo sana wa watendaji rasmi kwenye taasisi rasmi. Matokeo haya ya utafiti yanafanana na mawazo ya Benki ya Dunia (2017) kwamba kuna mapungufu kwenye michakato rasmi ya UW kwenye nchi nyingi zinazoendelea. Kimsingi matokeo haya ya utafiti yanaweza kutafsiriwa katika namna kuu mbili:

aibu kutokana na vitendo au mawzo ya kutenda kulingana na mila na desturi za jamii. Mila, na desturi kawaida zinakuwa na ushawishi kubwa kuhusu tabia na mienendo ya watu. Kwa pamoja mambo haya yaunda matitiki zinaoongoza tabia na utendaji wa taasisi umumia (Scott 2013a). Kwani sheria au sera peke yake siyo taasisi. Thamani yake inatokana na ushawishi wa pamoja wa vitu tofauti vinavyojenga tabia ya mtu. Kwa hiyo ili sheria au sera iwe na hadhi ya taasisi, inapaswa jingewe ulingo unaoingiza utambuzi wa desturi na utamaduni ili kusidia itekelezwe kikamilifu. Hii inahitaji pia kupwepo kwa misimbo ya kimaadili na kijamii kuhusu usahihi na uhalali wa vitendo vya watendaji na ukiukaji wake kuwa na athari kwa watendaji kisheria.

- i. **Moja**, maboresho yaliyojitokeza kwenye utoaji wa huduma za maji hayakutegemea mfumo rasmi wa ushirikishaji wa wananchi bali yaliwezesha na taasisi na taratibu nyingine kwa mfano msukumo uliotolewa na watendaji wasiokuwa rasmi walioshirikiana moja kwa moja na jamii.
- ii. **Mbili**, Pia haikaniki kwamba licha ya mfumo rasmi wa UW kutokuwa na msukumo mkubwa kutoka kwenye taasisi rasmi, umesaidia kutoa nafasi kwa wananchi kuhamasishana ndani ya jamii zao. Hoja hii inaungwa mkono na matokeo ya utafiti yanayoonyesha kwamba hatua za pamoja za wananchi zimetokana na uelewa wao wa pamoja wa misingi ya vikwazo vinavozikabili taasisi rasmi kwenye UW. Jamii zilipong'amua kwamba ushirikiano wao na watoa huduma unaweza usilite mafanikio yaliyotarajiwa, zilibun mifumo na njia mbadala za kuongeza nguvu na msukumo kwenye sera na sherai zilizopo.

Kwa hiyo ushahidi utokanao na utafiti unaonyesha kwamba utambuzi wa pamoja kati ya watendaji wa WATSAN kwamba uwekezaji wa kifedha ni muhimu kwenye kuleta mafanikio yenye tija kwenye WATSAN. Hii inamaanisha kwamba UW unachangia tu, na ukiachwa ujitegemee wenyewe hauwezi kuleta mafanikio tarajiwa. Wazo hili linajitokeza kwenye matarajio ya watendaji wa kitaasisi na kijamii ingawaje kiujumla mrejesho toka kwa wanajamii ni kwamba matarajiao yao hayakufikiwa. Licha ya kuhodhi upatikanaji wa taarifa kupitia UW, mamlaka za WATSAN zinaonekana hazina uwezo wa kukidhi mahitaji ya jamii. Hii inapunguza uwezekano wa ushirikiano wa jamii husika siku zijazo ambao ni kitendawili kwa sababu UW unalenga kuongeza la ushiriki wa jamii na uwajibikaji na sio kuhalalisha mikakati mbaadala inayokinzana. Katika hali hii uhalali wa maboresho ya sera ya WATSAN na kukubalika kwake unatiwa dosari na kuhatarishwa kutokana na mapungufu bainishwa ya UW.

Kwa hiyo kutakana na kutathmini kwa kina maboresho ya UW kama mchakato, utafiti huu umetoa mwanya wa kuelewa kwa kina changamoto za kisiasa na kiutekelezaji zitokanazo na kukubalika au kutokubalika na kusimamia sera ya ushirikishaji wa wananchi na matokeo haya ni muhimu tukizingatia yaliyosemwa na mwandishi Ole Therkildsen, kwamba ni lazima kutafuta , “jinsi ya kuboresha

na kuimarisha utendaji katika mazingira ya kiuchumi, kiutawala na kisiasa yaliyoko na yanayotabirika” (2000, uk. 20).

Hitimisho na Mapelelezo

Utafiti huu unaonyesha kwamba kwa ujumla ushirikishaji wa wananchi unatoa mchango mdogo sana kwenye mifumo inayoibuka kutoa huduma za WATSAN chini Tanzania. Hii inasababishwa na utata kwenye mfumo na michakato ya ushirikishaji (**Swali la Utafiti Na. 1**) jambo ambalo linachangia utata kuhusu jinsi gani UR inchangia kwenye kuboresha huduma za WATSAN (**Swali la Utafiti Na. 2**). Mwendelezo wa utata unadhirisha kutokuwepo jitihada za pamoja za kufanikisha zaidi UW na maboresho mengine kwenye WATSAN. Kuna umuhimu wa wadau hasa Serikali kurejea muundo wa taasisi za UW ili kupunguza utata huu na kuongeza umaalum, uwazi na uwekezaji wa rasimali utakaoweza kufanikisha malengo ya WATSAN. Hii itasaidia kurahisisha tafsiri ya sheria na kanuni zilizo rasmi na kuzioanisha na zile zisizo rasmi.

Maudhui ya utafiti huu na matokeo yake si msahafu juu namna ya kusanifu na kutekeleza maboresho ya kisera. Bali ni matokeo yanapaswa yazingatiwe katika jitihada za kutambua masuala muhimu kwenye utekelezaji wa sera za maboresho yanayostahili kurejewa na watendaji kwenye vyombo vya serikali na katika jamii wenye nia ya kuboresha utoaji wa huduma kwenye sekta ya WATSAN nchini Tanzania na kuimarisha sera ya ushirikishaji wa wananchi. Kutokana na matokeo haya, utafiti huu unatoa mapendekezo yafuatayo ya kisera yatakayoweza kuboresha utekelezaji wa dhana ya UW na kuimarisha utekelezaji wa maboresho ya sera ya Maji Safi na Maji Taka kwa ujumla:

- i. Ni muhimu mamlaka husika zikaboresha usanifu wa mifumo ya sheria na taratibu ili kuondoa mkanganyiko wa kisera.
- ii. Maboresho ya kisera ni muhimu yakatanguliwa na ubainishaji wa wadau husika na kuwapa kipaumbele katika utekelezaji ikiwemo uwezesaji wa rasilimali.
- iii. Ni muhimu maboresho ya kisera yakatoa kipaumbele kwa ufikiaji wa malengo halisia.
- iv. Ni muhimu kutazama upya dhana nzima ya UW katika muktadha mpana wa uchangiaji wa gharama na upanaji wa huduma kwenye sekta ya WATSAN.



REPOA

157 Mgombani/REPOA Street, Regent Estate

P.O. Box 33223, Dar es Salaam, Tanzania

Tel: +255 22 2700083, Cell: +255 75 409 1677 Fax +255 22 2705738

Website: www.repoa.or.tz Email: repoa@repoa.or.tz

Kituo cha Taarifa na Maarifa, REPOA

Kituo chetu cha Taarifa na Maarifa kinatoa mazingira mazuri kwa utafiti wa fasihi na vitabu / maandiko mbali mbali kwa haraka na kwa urahisi wa matumizi ya maarifa na taarifa. Imeanishwa na wavuti (internet) kwa ajili ya matumizi ya maktaba ya mkondoni (online) kuwasaidia wanaosomea Shahada za Uzamili na Uzamivu, watafiti na wasomi kwa kuwapatia magazeti, vitabu, ripoti n.k. ya siku za karibuni.

Saa za Ufunguzi

Kituo cha Taarifa na Maarifa kinakuwa wazi kuanzia Jumanne hadi Ijumaa saa 4.00 asubuhi hadi saa 7.00 mchana, saa 8.00 mchana hadi saa 11.00 alasiri. Maktaba ya mkondoni (online) ni wazi saa 24 kila siku.

@REPOA 2019

Matokeo, tafsiri, hitimisho, na maoni yaliyotolewa humu ndani ni ya mwandishi na siyo lazima yawe yanaakisi maoni na sera za REPOA.